Taarifa kwa wazazi wenye watoto na wanafunzi chekechea/ maangalizi baada ya shule/ shule ya kawaida

Chekechea/ maangalizi baada ya shule/ shule ya kawaida

Mtoto anaweza kuingia chekechea kuanzia umri wa mwaka mmoja. Katika shule ya kawaida, mtoto analazimika kuanza akifikisha umri wa miaka saba. Katika ratiba ya shule, mtoto anafundishwa masomo/ mada mbalimbali, anafundishwa kwa kutumia lugha ya Kiswidi na wanapata maelezo juu ya namna ya kuishi pamoja katika jamii.

Katika chekechea/ maangalizi baada ya shule/ shule ya kawaida nchini Uswidi, kuna wafanyakazi wa jinsia zote – wanaume na wanawake. Ni muhimu sana kuhakikisha kwamba mtoto/ mwanafunzi anafika katika shughuli na masomo yote ndani ya muda. Kama kuna tatizo lolote, ni wajibu wa wazazi kuhakikisha anawataarifu walimu husika kwanini mtoto/ mwanafunzi anashindwa kufika shuleni. Pia ni muhimu kwa wazazi kuhakikisha mtoto/ mwanafunzi anachukuliwa kutoka shule katika muda uliopangwa. Kama kuna mabadiliko yoyote katika muda, ni muhimu kwa wazazi kuwataarifu waalimu husika.

Wazazi pia wanatakiwa kuwapatia waalimu katika chekechea/ maangalizi baada ya shule/ shule ya kawaida namba za mawasiliano ya nyumbani, kazini au shuleni, na sio tu namba ya simu ya mkononi. Hii ni kuhakikisha kwamba wazazi wanaweza kupatikana kwa mawasiliano wakati wowote katika siku.

Utambulisho kabla ya kuanza chekechea

Katika wakati wa utambulisho kabla ya kuanza chekechea, wazazi wanatakiwa kuwepo. Utambulisho huu unachukua muda na ni hatua muhimu katika kujenga uhusiano kati ya chekechea, mtoto na wazazi.

Chakula

Katika chekechea/ shule ya kawaida, chakula kinachotolewa ni pamoja na chakula cha Kiswidi, chakula kwa wasiokula nyama, chakula kwa watoto wanatoka katika tamaduni na dini tofauti.

Shughuli za Nje

Mtoto/ mwanafunzi atashiriki katika shughuli za nje katika misimu yote ya hali ya hewa, hivyo mtoto/ mwanafunzi atatakiwa kuvalishwa nguo kulingana na hali ya hewa. Wazazi wanatakiwa kuacha nguo za ziada shuleni kwa ajili ya kubadilisha kama itahitajika.

Mkutano wa Wazazi na Waalimu

Mkutano wa wazazi na waalimu kuhusiana na maendeleo na mafanikio ya mtoto unafanyika kwa njia ya majadiliano kati ya waalimu, wazazi na mwanafunzi. Chekechea/ shule itahakikisha uwepo wa mkalimani kama atahitajika.

Kama kutakuwa na matatizo yoyote ambayo yanahitaji kujadiliana, muda utatengwa ili kukutana na mwalimu kutoka katika kundi la wafanyakazi.

Elimu ya Michezo

Katika chekechea/ shule, watoto na wanafunzi watashikiri katika michezo wakiwa na nguo mahususi na kuoga. Watashiriki katika siku za michezo na shughuli nyinginezo bila kujali jinsia.

Migogoro

Migororo inayojitokeza shuleni baina ya mtoto/mwanafunzi na wengine, kwanza kabisa, inasuluhishwa kwa kuwahusisha waliohusika katika mgogoro na kuongozwa na mtu mzima (mwalimu au mfanyakazi shuleni). Kama hatua hii haitosuluhisha mgogoro, ni wajibu wa chekechea/shule kuwahusisha wazazi wa mtoto na mtoto/mwanafunzi kujadili tatizo lililopo. Migogoro inayojitokeza nje ya muda wa shule haisuluhishwi na chekechea/shule.

Tabia

Katika chekechea/shule, mtoto/mwanafunzi anahitaji kuwa na lugha ya kistaarabu na tabia nzuri. Pia wanahitajika kuheshimiana.

Pia, tunahakikisha mazingira na vifaa vyote vinatunzwa vizuri katika chekechea/shule.

Kama kuna uonevu wowote wa kisaikolojia au kimwili, ni wajibu wa wafanyakazi kuijulisha Mamlaka ya Huduma za Jamii na Polisi. Adhabu yoyote ya kupiga (viboko n.k) ni kinyume na sheria za Uswidi na itaripotiwa au taarifa kufikishwa kwa mamlaka za sharia (polisi).

Kanuni za Msingi

Chekechea/ shule zinaongozwa kwa misingi ya kidemokrasia. Utakatifu wa maisha ya binadamu, uhuru wa kila mtu na uadilifu, thamani sawa kwa wote, usawa wa kijinsia, na mshikamano na walio dhaifu na wanaoishi katika mazingira magumu, ni maadili ya chekechea/shule.

Usawa/ Demokrasia

Chekechea/ shule zitakabiliana na mwelekeo na majukumu ya kijinsia ya kijadi. Tunawapatia watoto/wanafunzi (wakiume na wakike) fursa sawa na kuendeleza uwezo wao bila uwepo wa vikwazo na unyanyasaji wa kijinsia. Kila mtoto / mwanafunzi anapewa fursa ya kuunda na kuwa na mawazo yake wenyewe na kufanya uchaguzi na maamuzi kwa kuzingatia hali zao binafsi. Ushiriki na hali ya kujiamini katika uwezo wao vinaimarishwa na kukuzwa.

Mwonzozo wa Masaa 15

Mtoto ana haki ya kukaa chekechea / shule kwa masaa matatu kila siku au masasaa matano kwa siku tatu katika wiki, kama mzazi yeyote hana ajira, yuko katika mapumziko ya uzazi au likizo ya ugonjwa. Maamuzi ya idadi ya saa ya kuwepo shuleni ufanyika kwa kushauriana na Mkuu wa Shule na uzingatia maslahi ya mtoto na taasisi. Nyongeza yoyote ya muda inaweza tu kutolewa na Mkuu husika wa shule.

Mtoto Anayeumwa

Kama mtoto/mwanafunzi anaumwa ugonjwa wowote, ni lazima abaki nyumbani na asiende chekechea/shule. Kama mtoto/ mwanafunzi ataumwa wakati wa shule, ni muhimu kwa wazazi kuweza kupatikana/ kufikiwa na mapema iwezekanavyo, kufika shuleni kumchukua mtoto/mwanafunzi.

Msimu wa Joto/Jua (Summer)

Chekechea/ shule inachukukulia kwamba mtoto ubaki nyumbani wakati wa likizo ya wazazi. Mtoto/ mwanafunzi kuwa na likizo nje ya muda wa shule, baada ya kukaa muda mrefu katika kundi kubwa na wenzake, ina maana kubwa na umfurahisha. Kwa wiki moja katika mwaka, wazazi upewa fursa ya kuwa na muda binafsi na mwanafunzi kubaki chekechea/ katika maangalizi baada ya shule/ shuleni (kwa mfano wakati wa uwindaji wa Moose, likizo au ukarabati wa nyumba). Hii inafanywa kwa kushauriana na Mkuu na wafanyakazi/ shule. Hii wiki moja haiwezi kuwa wakati wa likizo ya shule.